

TANGAZO LA SERIKALI NA. 205 la tarehe 1/8/2003

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982

(NA.9 YA 1982)

SHERIA NDOGO

**Zimetungwa chini ya vifungu vya 13 na 15(c)
SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA
YA MOSHI (KODI YA MAJENGO) 2003**

Jina na tarehe kuanza kutumika. 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi (Kodi ya Majengo) za 2003 na zitaanza kutumika tangu tarehe 1 Januari 2003 na zitatumika katika eneo lote lililopo katika Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

Tafsiri 2. Katika Sheria Ndogo hizi: -
“Daftari la Uthamini” maana yake ni daftari lenye orodha na thamani ya nyumba zilizofanyiwa uthamini mwaka 2002 na taarifa ya kukamilika kwake kutangazwa katika Gazeti la Serikali

“Halmashauri” ina maana ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

Tangazo Na 305 la tarehe 26/6/2002. “Jengo” ina maana ya mali isiyohamishika iliyopo kwenye kiwanja ikiwa ni pamoja na kiwanja ambacho hakijaendelezwa Inayotozwa kodi kwa mujibu wa Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa na Sheria ya viwango.

“Kodi” maana yake ni ada itozwayo kulingana na thamani ya kila jengo.

“Mkurugenzi” ina maana ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

“Muda wa Malipo” ina maana ya muda wa kulipa kodi ya Jengo.

“Sheria” ina maana ya Sheria za Viwango na Fedha za Serikali za Mitaa.

“Tathimini” maana yake ni tathimini ya kodi inayofanywa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Sheria Na.2 ya 1983. Na. 9 ya 1982 “Uthamini” Maana yake ni uthamini iliyofanyika ili kujua thamani ya jengo Iliyofanywa na kuingizwa kwenye daftari la Uthamini kwa mujibu wa Sheria

Wajibu wa kulipa kodi 3. Mtu yeyote anayemiliki jengo lililopo katika eneo la Halmashauri ambalo limefanyiwa au halijafanyiwa uthamini ana wajibu wa kulipa Kodi ya Jengo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Muda wa Kulipa Kodi 4. Kuanzia tarehe 1 ya Januari hadi tarehe 31 ya Machi kwa kila mwaka utakuwa ndiyo muda wa kulipa Kodi ya Jengo inayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Riba kwa malipo yaliyochelewa 5. Inapotokea kwamba mmiliki wa jengo au Msimamizi wake akashindwa kulipa kodi ya Jengo katika muda wa kulipa kodi, atatozwa riba ya asilimia Moja (1%) kwa Mwezi hadi atakapolipa deni lake kama ilivyoelekezwa na Sheria

Ubambuzi kwa mali za waliyoshindwa kulipa kodi 6. Itakuwa ni haki kwa Halmashauri kukamata na kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa wa kodi ya Jengo iwapo watashindwa kulipa kodi ndani ya muda wa kulipa kodi hiyo na kama ilivyolekezwa kwenye Sheria ya Uthamini.

7. (1) Bila ya kuathiri haki na mamlaka mengineyo, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumwamuru mtu yeyote aishie katika jengo ambalo mmiliki wake hayupo katika eneo la Halmashauri, kutoa taarifa kuhusu jengo hilo au malipo yoyote ambayo mmiliki wake anastahili kulipa kwa Halmashauri.

(2) Pia Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kukamata mali zinazohamishika za mmiliki wa Jengo bila ya kujali kuwa mali hizo hazikukutwa katika Jengo linalostahili kulipiwa kodi hiyo.

Adhabu na Makosa 8. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo: -

(a) Mmiliki wa jengo atakwepa au atajaribu kukwepa kulipa kodi anayotakiwa kulipa.

(b) Mkazi yeyote wa Jengo atakataa au atajaribu kukataa kutoa taarifa kuhusu mmiliki wa jengo.

(c) Mkazi yeyote wa kwenye jengo atakataa au atajaribu kukataa kutii agizo la kutoa malipo ya kodi .

(a) Mtu yeyote atazuia au atajaribu kumzuia mtumishi au wakala wa Halmashauri kuingia kwenye jengo kwa ajili ya kukusanya kodi au kukamata mali inayohamishika.

Na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Elfu Ishirini au isiyozidi Shilingi elfu Hamsini au kutumikia kifungu cha miezi sita au kulipa faini na kutumikia kifungu jela kwa pamoja.

Kufutwa kwa GN Na.777 ya 1987 9. Sheria Ndogo za Halmashauri ya Mji wa Moshi (The Moshi Town Council Property Rate) By-Laws 1987) pamoja na marekebisho yake yote zimefutwa.

JEDWALI

Aina ya majengo	Kodi inayotakiwa kulipwa
1.Majengo yote yaliyofanyiwa uthamini	asilimia 0.12% kwa mwaka ya thamani ya jengo kama inavooneshwa Kwenye daftari la uthamini lakini siyo chini ya Shilingi 5,000/=.
2.Majengo ya Kudumu yaliyopo katika maeneo yasiyopimwa na hayajafanyiwa uthamini	Shilingi 7000/= kwa mwaka .
3.Majengo ya muda yaliyopo katika maeneo yasiyopimwa na hayajafanyiwa uthamini .	Shilingi 6000/= kwa mwaka
4.Majengo yanayokaliwa na wamiliki bila ya wapangaji .	Shilingi 6,000/= kwa mwaka.

Mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi umewekwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 06/06/2003 na kubandikwa mbele ya: -

L. S. TARIMO
Mstahiki Meya
Halmashauri ya Manispaa ya Moshi

S. Z. Muyinga
Mkurugenzi
Halmashauri ya Manispaa ya Moshi

NAKUBALI

MHE. BRG. JEN MSTAAFU H.A.H. NGWILIZI,
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za
Mikoa na Serikali za Mitaa

DODOMA
4 Julai, 2003